# Usemezanoghaibu katika Diwani ya *Kimbunga*

*Mohammed Soud Juma*
*Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA)*

**Ikisiri**

**Makala haya imekusudia kushughulikia usemezanoghaibu unaojitokeza katika diwani ya *Kimbunga*, iliyoandikwa na Haji Gora. Aidha, makala imejikita katika kuangalia aina za usemezano uliotumika katika mashairi ya msanii huyo. Pia, makala inaonesha aina mpya ya usemezano iliyotumiwa na msanii huyu, kinyume na aina zile zilizoorodheshwa na Bakhtin juu ya aina za usemezano zinazotumika katika riwaya na kuonesha uwezekano wa kutumika kwa usemezano na usemezanoghaibu katika uga mwengine wa fasihi kinyume na riwaya peke yake. Hivyo, makala inaonesha kutumika kwa usemezano katika ushairi wa Kiswahili na kuibuka kwa usemezanoghaibu, kuwa ni dhana mpya ya usemezano inayopatikana kwa wasanii wa fasihi hasa wasanii wa ushairi. Katika makala haya inapendekezwa kufanyike kwa utafiti mwengine kwa kuitumia dhana ya usemezanoghaibu na kuzama ndani zaidi ili kuweza kugundua mambo mapya yanayotumiwa na wasanii.**

**Maneno Muhimu:** Usemezanoghaibu, Diwani, Kimbunga, Usemazano.

## Utangulizi

Makala haya inashughulikia juu ya usemezanoghaibu unaojitokeza katika diwani ya *Kimbunga* iliyoandikwa na Gora (1994). Diwani hii ya *Kimbunga* inazungumzia juu ya mawaidha mbalimbali kuhusiana na maisha ya wanadamu katika kulifikia suala zima la ujenzi wa jamii mpya. Msanii kupitia maudhui ya diwani yake, anatoa maonyo na maadili mbalimbali kwa kutumia mbinu mbalimbali za kisanaa. Miongoni mwa mbinu hizo, msanii ametumia usemezano kama njia mojawapo ya kufikisha ujumbe alioukusudia.

Usemezano ni dhana inayotumika katika kazi za fasihi kwa ajili ya kueleza mahusiano yaliyopo kati ya matamko mbalimbali, matamko hayo ni yale yanayotumiwa na wasanii hao wakati wa kuwasilisha maudhui yao. Usemezano kama nadharia ya kifasihi, inahusishwa na mtaalamu wa Kirusi aitwaye Mikhail Mikhailovich Bakhtin aliyezaliwa mwaka 1895, ambaye ndiye muasisi wa nadharia hii, naye ameitumia katika kueleza uhusiano unaopatikana kati ya matamko mbalimbali. Nadharia ya usemezano huona kwamba kila tamko huwa na athari ya matamko mengine yaliyotangulia au yatakayofuata, yaani matamko yaliyotangulia huchochea tamko au matamko ya baadaye (Wamitila, 2003:262). Usemezano sio lazima uhusishe wazungumzaji wawili, badala yake, sifa ya usemezano ule wa kifasihi unahusisha maana kadhaa zinazoweza kubadilikabadilika kwa kutegemea muktadha, hali, wakati, na wahusika. Hivyo, kunaibuka dhana mbalimbali zinazohusiana na usemezano.

Hivyo, tunaweza kusema kuwa usemezano ni mtagusano wa wasanii wawili wakijibizana papo kwa papo. Pia, upo usemezano wa mtu na nafsi yake na hata usemezano wa mtu mmoja na mtu mwingine ambaye yuko mbali naye, ambao tunauita usemezano-ghaibu (usemezano wa nje): kwa mujibu wa BAKIZA (2010) wanaeleza "ghaibu ni hali ya kutojulikana au kutoonekana jambo au kitu bayana". Yaani kwa hapa ni msanii mmoja akisemezana na msanii aliyekuwa yuko mbali naye. Hii inaingia hata shairi moja likisemezana na shairi lingine kupitia miktadha mbalimbali. Na kwa usemezano huo wa ghaibu, mtafiti ameweza kuibua kitu kipya katika dhana ya usemezano, na kuuita usemezanoghaibu.

## Usuli wa Mwandishi wa Diwani ya *Kimbunga*

Mwandishi wa diwani ya *Kimbunga* ni Haji Gora Haji, ambaye amezaliwa Zanzibar mwaka 1933 huko kisiwani Tumbatu katika kijiji kidogo cha Kokoni kilichoko katika kisiwa hicho cha Tumbatu.

Wazazi wake walimpeleka mjini katika mtaa wa Mkunazini, wakati akiwa na umri wa miaka mitano kwa ajili ya malezi, na akakulia huko.

Akiwa mjini, alipelekwa chuoni kwa ajili ya kusoma dini ya kiislamu. Haji Gora hakuwahi kupelekwa skuli, kwani alikuwa akifanyakazi tokea utotoni mwake. Alifundishwa kazi mbalimbali hasa kazi za baharini, zikiwemo za uvuvi wa nyavu, uvuvi wa madema kupitia mjomba wake, Haji Mjumbe na kupitia baba yake mdogo, Bwana Pandu Haji.

Alipokuwa na umri wa miaka 16, alijiunga na kikundi cha vijana huko Tumbatu, kikundi hicho kulijulikana kwa jina la 'Ujinga Mewing'. Wanakikundi hao walijishughulisha na ngoma, ambapo huwa wanashindana na vikundi vyengine vya ngoma kwa kutungiana mashairi na kutambiana hadharani, kulumbana na kujibizana kwa njia ya utambaji wa mashairi. Utambaji huo ndio uliompelekea kuwa gwiji na mahiri wa utungaji wa mashairi.

Katika uga huu wa ushairi, Haji Gora mbali na kuandika diwani hii ya *Kimbunga* lakini pia ameandika baadhi ya vitabu vikiwemo *Siri ya Ging'ingi, Ujanja wa Sungura, Nahodha Chui, Maisha ya Haji Gora, Shuwari,* na *Utenzi wa Visa vya Nabii Suleiman bi Daud (AS).*

**Mapitio ya Kazi Tangulizi**

Waandishi mbalimbali wameandika kuhusu usemezano katika kazi za fasihi. Miongoni mwao ni Suter (2017), ambapo alichunguza aina za usemezano zinazojitokeza katika diwani ya *Sikate Tamaa* (1980), iliyoandikwa na Said Ahmed Mohamed. Aidha, Suter amebainisha namna vipengele vya usemezano vinavyokuza dhamira na maudhui katika diwani hiyo. Kwa mfano usemezano katika shairi la *Mwanakupata* ambapo mwandishi ameonesha majibizano ni sehemu ya usemezano kama anavyoeleza Bakhtin (1981, 1984) kuwa dhana ya majibizano inajitokeza katika utanzu wa riwaya. Hata hivyo, Wamitila (2002) amekuja na ukengeushi wa nadharia ya Bakhtin na kudai kuwa usemezano wa majibizano hujitokeza pia katika ushairi kinyume anavyodai Bakhtin. Maelezo haya ya Wamitila (ameshatajwa) yamemsaidia mtafiti kuweza kugundua pengo la utafiti na kuweza kuiangalia dhana hii ya usemezano katika mashairi kwa jicho la upembuzi na kuweza kuibua aina za usemezano katika diwani ya *Kimbunga,* pia kuweza kuibua aina mpya ya usemezano, ijulikanayo kama ni usemezanoghaibu kutoka katika diwani hiyo.

Aidha, Njogu (1993) naye pia amekuja na ukengeushi wa nadharia juu ya madai ya Bakhtin ya kuwa utanzu wa riwaya ndio utanzu bora zaidi katika nadharia ya usemezano kwa madai ya kuwa, ushairi hubeba uzungumzi wa mtu mmoja tu. Njogu anaendelea kufafanua kuwa ushairi ni wa kisemezano, kwani ndani yake kunakuwepo na majibu ya usemi uliotangulia au muendelezo wa mazungumzo yanayofuata. Akitolea mfano wa shairi la Al-inkishafi. Uchunguzi huu wa Njogu umeweza kumsaidia mtafiti katika kulithibitisha dai lake kwa kuoesha usemezano ndani ya mashairi ya diwani ya *Kimbunga.*

Mwita (2018), katika tasnifu yake kwa ngazi ya umahiri. Yeye alichunguza usemezano katika tamthiliya ya Kiswahili, ambapo alifanya ulinganishi wa dhana hii kupitia tamthiliya ya *Mashetani* na *Pambo*. Katika utafiti wake alibaini kuwepo kwa vipengele vya usemezano katika kazi za tamthiliya na kutilia mkazo maneno ya Bakhtin ya kuwa usemezano ni wa mazungumzo ya kidaiolojia kama ilivyo katika tamthiliya. Pamoja na kuwa utafiti wa Mwita (ameshatajwa) umehusisha tamthiliya, lakini umeweza kumsadia mtafiti katika kubaini aina za usemezano zilizojitokeza katika tamthiliya hizo, pia zimeweza kujitokeza katika diwani ya *Kimbunga*, hivyo utafiti umeweza kuthibitisha kuwa usemezano upo hadi katika mashairi.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), majibizano ndiyo jambo ambalo linalohuisha usemezano baina ya wahusika. Na ndio maana Bakhtin akatilia mkazo kuwepo kwa usemezano katika uga wa tamthiliya, kwani wahusika wake huwa wanasemezana kwa njia ya majibizano. Kutokana na kigezo hiki, mashairi ya *Kimbunga* yameonekana kuwemo ndani yake majibizano ya wahusika ama ya washairi tofauti au kwa shairi moja. Kupitia usemezano huo wa kujibizana kwa wahusika ama kwa washairi, ndipo dhana hii iliweza kumsaidia mtafiti kugundua aina nyingine ya usemezano, ambao ni usemezanoghaibu.

Mtimbo na Suleiman (2004) wamefanya uchambuzi kuhusu mashairi ya *Kimbunga* na kubaini dhamira mbalimbali zinazojitokeza katika diwani hiyo. Dhamira hizo ni kama malezi, wusia na uongozi bora, ambazo hujitokeza kwa wingi katika mashairi ya Haji Gora. Aidha, Njogu na Chimerah (1994), katika kitabu chao cha *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu.* Wameitaja tu diwani ya *Kimbunga* kuwa ni diwani bora ambayo inazingatia urari wa vina na mizani. Kupitia uchambuzi huo wa mashairi ya *Kimbunga* umeweza kumsaidia mtafiti kuibua aina za usemezano zilizojikita kwenye diwani hiyo kupitia dhamira mbalimbali.

Naye Hassan (2013), katika tasnifu yake ya kuchunguza vipengele vya fani katika mashairi ya Kiswahili. Amewalinganisha Haji Gora (1994) na Kezilahabi juu ya ushairi wao kupitia diwani ya *Kimbunga* na ushairi wa Kezilahabi kupitia diwani zake mbalimbali. Katika tasnifu yake hii, amebaini kuwa kuna kutofautiana kwa vipengele vya fani katika ushairi wa wasanii hawa teule. Aidha, hata dhamira zao zimeweza kutofautiana kwa kiasi fulani. Hivyo, kwa uchambuzi wa dhamira hizo umeweza kutoa mchango mkubwa wa makala haya kwa kuibua usemezano unaojitokeza katika diwani ya *Kimbunga* kupitia dhamira hizo. Kwani ndani ya dhamira ndimo zilizoibuliwa aina za usemezano.

Uchambuzi wa data za makala haya umefanyika kupitia nadharia ya usemezano. Nadharia ya usemezano imeasisiwa na mwanataaluma wa Kirusi aitwaye Mikhail Mikhailovich Bakhtin (1895 – 1975). Wanashule ya Bakhtin hawakuvutiwa na dhana za kiisimu zinazoiongoza misingi ya nadharia za kimuundo, na ndipo wanashule hao, wakaja na dhana hii ya usemezano iliyoshughulikia lugha au diskozi kama ni kitu cha kijamii. Baadhi ya wataalamu waliounga mkono nadharia hii na kuifafanua kwa kina zaidi ni pamoja na Lodge (1990) na Dentith (1995). Katika nadharia hii, Bakhtin anaeleza kwamba usemi wowote huwa unajibu kile kilichopo, kilichopita na hata kile kinachotarajiwa kusemwa baadae. Msanii wa diwani ya *Kimbunga* huwasilisha usemi katika tungo zake wenye kujibu kilichosemwa, kinachosemwa, na hata kitakachosemwa. Aidha, anaendelea Bakhtin kuwa, dhana ya usemezano haina maana ya mazungumzo ya moja kwa moja au ya ana kwa ana kati ya wahusika wawili kama inavyojitokeza katika tamthilia, ngonjera au mazungumzo ya dailojia. Na si lazima usemezano uhusishe wazungumzaji wawili. Kwa hiyo, ndivyo tunavyoweza kupata aina mbalimbali za usemezano kupitia mashairi.

Hivyo, nadharia hii ya usemezano ilimsaidia mtafiti katika kuainisha usemezano wa mshairi uliojitokeza katika diwani ya *Kimbunga.* Aidha, nadharia ilimsaidia mtafiti katika kuainisha aina mbalimbali za usemezano ndani ya mashairi, pamoja na kubainisha usemezano wa ndani ya mashairi (yaani mashairi yenyewe kwa wenyewe) na ule usemezanoghaibu (wa nje) uliojitokeza katika diwani hii kwa kusemezana na mashairi mengine yaliyonje ya diwani hii.

Licha ya kuwa nadharia ya usemezano kwa mtazamo wa Bakhtin, inaonesha uzungumzi nafsi ni sehemu moja wapo ya usemezano. Hata hivyo, ughaibu unadhihirika pale msanii anapozungumza na moyo wake juu ya maswaibu mbalimbali. Kupitia uzungumzi huo, nadharia ya usemezano inakwenda mbele zaidi kwa kuibua usemezanoghaibu ndani ya ushairi wa Kiswahili.

Uchunguzi umebaini kuwa dhana ya usemezanoghaibu imejengeka kwa sifa zifuatazo:-

a. Matumizi ya nafsi ya tatu.

b. Matumizi ya nafsi ya pili.

c. Msanii kuzungumza na moyo (nafsi) yake.

Kupitia sifa hizo ndani ya diwani ya Haji Gora, mtafiti ameonesha huo usemezanoghaibu kama ni moja ya dhana ya usemezano inayodhihirika kupitia ushairi wa Kiswahili.

Utafiti unajishughulisha na usemezanoghaibu unaojitokeza katika ushairi wa Kiswahili kupitia diwani teule. Diwani hii inaonekana kama inazungumzia juu ya mawaidha kuhusiana na maisha ya wanadamu katika kulifikia suala zima la ujenzi wa jamii mpya. Mwandishi kupitia maudhui ya diwani yake, anatoa maonyo na maadili mbalimbali kwa kutumia mbinu mbalimbali za kisanaa. Miongoni mwa mbinu hizo ni usemezanoghaibu, ambao umetumika kama njia ya kufikisha ujumbe.

Kwa mtazamo huo wa Bakhtin pamoja na wataalamu mbalimbali walioshughulikia dhana ya usemezano katika fasihi ya Kiafrika, unaonesha kuwa usemezano upo katika kazi za kifasihi za kimaandishi kwa kuhusisha kauli mbili za kusemezana kati ya msemeza na msemezwa. Hata hivyo, hawakujihusisha na msemezano wa mtu wa tatu (usemezanoghaibu). Kwa hivyo, utafiti huu unajikita katika kazi za kifasihi kwa upande wa ushairi na kushughulika na diwani ya Haji Gora, unaangalia dhana nyengine ya usemezanoghaibu ndani ya nadharia ya usemezano inavyobainika katika ushairi wa Kiswahili.

**Mbinu za Kukusanyia Data**

Mbinu iliyotumika katika kukusanyia data za utafiti huu ni mbinu ya maktabani, mtafiti alianza kuipitia nadharia ya usemezano kutoka katika maandiko mbalimbali. Kisha, akadurusu diwani ya *Kimbunga* kwa umakini zaidi kwa kuzingatia kiunzi cha nadharia. Ambapo data zilizopatikana ziliweza kuoanishwa na kiunzi cha nadharia, na hatimaye kuibua aina za usemezano kutoka diwani hii pamoja na usemezanoghaibu.

**Uchambuzi wa Data**

Uchambuzi wa data umefanywa wa kimaelezo, umeonesha kuwepo kwa usemezano katika diwani ya *Kimbunga*. Kutokana na misingi ya usemezano kama inavyoorodheshwa na Bakhtin kupitia vipengele kumi. Mtafiti ameweza kuibua usemezano kupitia vipengele hivyo, navyo ni pamoja na uzungumzi nafsi, majibizano, tamko ni jibu la tamko jengine, uwingi sauti, kronotopu, utendaji, usimulizi wa kisanaa, kani pewa na kani kitovu, sajili mbalimbali, kanivali, na mwishowe usemezanoghaibu.

**Uzungumzi Nafsi**

Uzungumzi nafsi ni kipengele cha usemezano, ambapo mtu/msanii husema na nafsi yake. Kwa mujibu wa Mukarovsky (1977), anaeleza kuwa, uzungumzi nafsi ni namna mojawapo ya usemezano. Hii ni kwa sababu mtu anakuwa anasema na nafsi yake. Aidha, Biersteker (1996), yeye anaeleza kuwa namna ambavyo wasanii wengi wa karne ya ishirini wameathiriwa na Muyaka kaupitia shairi la ‘Moyo’ ambapo msemaji ni moyo, na hapo moyo unasemezana na nafsi. Hapa tunapata picha ya moyo unasema na nafsi juu ya kile inachokitamani. Katika diwani hii ya *Kimbunga* mshairi amedhihirisha kuwepo kwa usemezano katika diwani yake, kwani ametumia kipengele cha uzungumzi nafsi, kwa kuizungumza nafsi yake juu ya ngoma ya beni na namna anavyoistaajabia juu ya uchezaji wake. Mfano katika shairi la *Beni*, ubeti wa kwanza, mshairi (mzungumzaji) anajiuliza nafsi yake juu ya ngoma ya beni na kuishangaza nafsi yake kwa ngoma hiyo.

*1.* *Mimi inanishangaza,* *beni ya mbwa kachoka*
*Wala sitojipumbaza, karibu yake kufika*
*Baada ya kuchunguza, tufikirie haraka*
*Shuruti utowe haya, ndio uicheze beni*

Kupitia mfano huu unatuonesha namna msanii alivyoweza kutumia kipengele cha uzungumzi nafsi katika usemezano. Kwani ameweza kuisemeza nafsi yake juu ya jambo linalomtatiza katika nafsi yake. Mfano pale aliposema *‘**Mimi inanishangaza**…’*

Aidha, katika shairi la *Paka* msanii ametumia usemezano wa uzungumzi nafsi kwa kutumia nafsi ya kwanza pamoja na nafsi ya tatu. Mfano kutoka katika ubeti wa kwanza.

1. *Paka nakuasa wizi, wacha kuiba samaki*
*Imekuwa yako kazi, majikoni huondoki*
*Haufai uchokozi,  si kizuri kitu hiki*
*Paka nakuasa wizi, vitoweo usiibe*

Kupitia mfano huu, msanii ametumia njia niengine ya uzungumzi nafsi kwa kusema na nafsi yake kwa kusudio la kumwambia mtu wa tatu/nafsi ya tatu, lakini mtu huyo hayupo na wala hatafahamu kwa lile analoambiwa. Kwa kuchukuwa taswira ya paka kuzungumza nae, ambapo ni sawa na kuiambia nafsi yake mwenyewe. Mfano pale aliposema ‘***Paka nakuwasa wizi, wacha kuiba samaki…***’.

Pia katika shairi la *Bahati,* msanii ametumia mbinu ya usemezano wa uzungumzi nafsi kwa kuzungumza na nafsi yake juu ya suala zima la kupewa nafasi ya kuchagua kati ya bahati na mali. Uzungumzi huo wa nafsi umekuja kwa kutumia nafsi ya kwanza umoja kama ni kiashirio cha kuzungumza na nafsi yake. Mfano kutoka katika ubeti wa kwanza.

1. *Kama nitahiyarishwa, penye viwili teuwa*
   *Mali nikiamrishwa, au bahati chukuwa*
   *Sitongoja kuoneshwa, bahati nitanyakuwa*
   *Bahati ni kitu bora, kiumbe akijaliwa*
   *Ijapokuwa fukara, yake hwenda kwa muruwa.*

Katika mfano huu, tunaona kwamba msanii ametumia uzungumzi nafsi kama ni mbinu ya usemezano kwa kuzungumza na nafsi yake kwa kutumia nafsi ya kwanza umoja. Mfano ni pale aliposema '*Kama **ni**tahiyarishwa… Mali **ni**kiamrishwa… bahati **ni**tanyakuwa'.*

**Majibizano**

Majibizano ni hali ya mtu mmoja au kikundi cha watu wakijibizana, ama kwa kuuliza swali na mtu mwengine akajibu au kwa kushiriki moja kwa moja katika mazungumzo kwa kuchangiana mawazo kwa kupishana kimazungumzo. Kwa upande wa fasihi, majibizano ni aina ya usemezano, ambapo msanii mmoja huwa anazungumza na msanii mwengine kwa njia ya kujibizana moja kwa moja kwa kupeana nafasi katika mazungumzo yao, mfano mzuri ni utungo wa ngonjera. Aidha, katika utanzu wa ushairi katika kipera cha nyimbo, tunapata majibizano kupitia nyimbo za taarabu. Mfano katika wimbo wa '*Sibalkheri mpenzi'* waimbaji wawili; Mwapombe Hiari na Sami Haji Dau wakisemezana kwa njia ya majibizano, ambapo ni kinyume na utaratibu uliozoeleka wa uimbaji wa taarabu. Pia majibizano hutokea kwa msanii mmoja akijibizana na msanii mwingine kupitia shairi. Au hata kutoa majibu au kuuliza swali kwa njia ya shairi ili msanii mwingine aweze kujibu swali lililoulizwa kishairi. Hata hivyo, katika diwani ya *Kimbunga* usemezano wa majibizano umejitokeza kwa njia ya usemezanoghaibu, yaani msanii akisemezana na msanii mwingine aliye mbali na yeye. Mfano ni shairi la *Kipaji* katika ubeti wa kwanza.

*1. Rafiki yangu Mvungi, Nakanusha usemayo*
   *Kwako mkono siungi, Nakueleza yaliyo*
   *Kipaji ndio msingi, Jitihada kichocheyo*
   *Juhudi kisaidiyo, Ushairi ni kipaji*

Kupitia shairi hili msanii ameonesha namna kipengele cha majibizano kuwa ni sehemu ya usemezano. Msanii ameweza kutuonesha jinsi akisemezana na mtu mwengine akiwa mbali na yeye. Usemezano wa aina hii wa kujibizana, tunauita usemezanoghaibu. Kwani msanii anasemezana na msanii mwengine ambaye ni Mvungi, ambaye kwa hapo yuko mbali naye.

Pia shairi la *Usimpige mkeo*, msanii ameonesha namna anavyojibizana na mtu mwengine kwa njia ya usemezanoghaibu wakati akitoa mafunzo na maadili ya kuishi vyema na mke. Mfano ubeti wa pili.

*2. Umemchukua kwao, waliko wazazi wake*
   *Umpe kula na nguo, na vizuri umuweke*
   *Usimpe masumbuo, huo si wajibu wake*
   *Kupiga piga si kwema, kaa nae kwa salama*

Kutoka katika data ya shairi hili la *Usimpige mkeo*, inadhihirisha kuwepo kwa usemezano ambao tunauita **usemezanoghaibu**. Kwani msanii anazungumza na mtu mwengine ambaye hayupo hapo, ila akimpa nasaha njema za kuishi vizuri na mke wake na ajiepushe na tabia ya kumpiga mke. Usemezano unadhihirika kwa njia ya majibizano, ni pale aliposema '***Umemchukua kwao****…'* hii inamaanisha nafsi ya msanii ikijibizana na nafsi ya mtu wa tatu ambaye haonekani hapo.

**Tamko ni Jibu la Tamko Jengine**

Kuwepo kwa tamko la msanii likijibu tamko la msanii mwengine. Ni aina ya usemezano ambao wasanii huwa wanasemezana kupitia tungo zao. Yaani utungo mmoja unakuwa ni jibu kwa utungo

mwengine. Na hii ni moja kati ya aina za **usemezanoghaibu**. Na pia kupitia kipengele hiki ndani yake tunapata kipengele cha kuathiriana na maandishi mengine. Yaani shairi moja ama msanii mmoja huathiriwa na utunzi wa msanii mwengine na hivyo kunadhihirisha kuwapo kwa usemezano katika mashairi. Mfano katika shairi la Al-inkishafi kuna mwangi katika mashairi mengi ya Kiswahili ya Afrika ya Mashariki kwa kuanza na kumshukuru Mungu au kumsifu Mungu Muumba. Msanii wa *Kimbunga* ametumia usemezano wa aina hii kwa kutoa majibu ya tungo zilizotangulia. Mfano shairi la *Kipaji* ubeti wa kwanza.

1. *Rafiki yangu Mvungi, Nakanusha usemayo*
*Kwako mkono siungi, Nakueleza yaliyo*
*Kipaji ndio msingi, Jitihada kichocheyo*
*Juhudi kisaidiyo, Ushairi ni kipaji*

Katika mfano huo, tunaona namna msanii anavyotoa jibu kwa msanii mwengine baada ya utungo wa msanii wa kwanza (Mvungi) kueleza kuwa ushairi ni jitihada aliyonayo mtu katika kutunga mashairi.

Aidha, katika shairi la *Kiswahili* msanii ameonesha **usemezanoghaibu** kupitia kipengele cha tamko lake likiwa ni jibu kwa tamko lililotangulia. Hili limekuja kujibu wale wanaodai kuwa Kiswahili hakina mwenyewe bali kimezuka tu. Mfano katika ubeti wa kwanza.

1. *Nimeifunga safari, kukufatia kwa mbali*
*Ili kuja kuhubiri, jibu la lako suali*
*Ingawa muhutasari, tia ndani ya akili*
*Lugha hii Kiswahili, wenyewe ni wa Mwambao*

Kupitia data hii, msanii ametoa majibu ya swali lililoulizwa na wasanii wengine juu ya wenye kumiliki lugha ya Kiswahili na kuonesha kwa njia ya majibu yake kuwa Kiswahili kina wenyewe ambao ni watu wa mwambao. Pale aliposema '***Ili kuja kuhubiri, jibu la lako suali… Lugha ya Kiswahili, wenyewe ni wa mwambao'.***

Pia katika shairi la *Kasa,* msanii ametumia **usemezanoghaibu** kwa kupitia kipengele cha tamko ni jibu la tamko jengine, ambapo msanii wa *Kimbunga* ameanza kutoa tamko kwa kutegemea kupata jibu kwa wasanii wengine kupitia suali alilouliza. Mfano ubeti wa pili.

2. *Nijibuni marafiki, msinitie kapuni*
*Hayo ndiyo mashukuki, yalonikaa moyoni*
*Kama linalo wafiki, haraka nijulisheni*
*Vipi tunamsadiki, mnyama au samaki*

Kupitia data hizi, inaonesha ni wazi kuwa msanii ametumia vyema kipengele cha usemezano katika diwani yake. Kwani, kwa kutoa majibu ya suala liloliulizwa na washairi wengine juu ya wamiliki wa lugha ya Kiswahili. Na pia kwa kuuliza swali la kutaka kumjua kasa bila ya kumuainisha ni nani anayetaka atoe majibu, pale aliposema *'**Nijibuni marafiki, msinitie kapuni… Vipi tunamsadiki, mnyama au samaki**'*. Ni dhahiri kuwa ni usemezanoghaibu katika kipengele cha usemezano kwani anayeulizwa hakumtaja kwa jina wala kumuainisha, bali yeyote anayeweza kutoa majibu anaweza kumjibu.

**Uwingi Sauti**

Katika kazi za mashairi huwepo na sauti nyingi tofauti tofauti ambazo ziko huru. Wahusika huwa na sauti zilizo na mamlaka sawa na sauti ya msimulizi ambayo inahusika katika usemezano na sauti za wahusika wengine. Sauti haziwezi kurejelea msemaji peke yake bali hurejelea yale mahusiano ya nguvu yanayoathiri na kumuweka msomaji katika hali fulani. Kipengele hiki hakijatumika katika diwani ya *Kimbunga*.

**Kronotopu**

Kronotopu ni matukio yanayotimbwa hasa katika mpito wa wakati na mahali fulani. Yaani ni kurejelea kazi za kifasihi zinazoweza kuvuka mipaka ya mahali na wakati na huakisi mipaka ya

kidhahania. Kupitia kipengele hiki, msanii ameweza kulibainisha jambo hili katika shairi la *Uchawini,* katika ubeti wa kwanza.

1. *Nilipokwenda Ging'ingi, huko niliyoyaona*
   *Kuna watu moja rangi, sura zashabihiana*
   *Bali hayana msingi, wanayofanyiziana*
   *Haweshi kusokotana, kila mmoja ni yeye.*

Aidha, katika shairi la *Kitendawili*, msanii ameonesha usemezano kupitia kipengele cha kronotopu kwa kurejelea matukio yanayoweza kuvuka mipaka na mahali halisi na kuakisi mipaka ya kidhahania. Mfano katika ubeti wa kwanza.

1. *Kitendawili natega, nategа kiteguweni*
   *Teguweni bila woga, na kutaja kwa lisani*
   *Paa mayai kataga, katotoa wana nyani*
   *Wateguzi tegueni, moja baada ya moja.*

Kupitia shairi hili msanii ameweza kuonesha usemezano katika kipengele cha kronotopu kwa kuingiza katika kazi yake mambo yaliyovuka mipaka ya kiuhalisia na kwenda kwenye mipaka ya kidhahania, kwani sehemu inayoitwa **Ging'ingi** inasadikiwa kuwa ipo, ila haionekani kwa macho ya kawaida. Yaani ipo kwa jicho la kimazingara. Pia msanii ameonesha mambo yaliyovuka mpaka katika akili za binadamu; pale aliposema: ***'Paa mayai kataga, katotoa wana nyani'***, kwa kumtaja mnyama paa ambaye ni mwenye sifa ya kuzaa, lakini msanii akasema kuwa ni mwenye kutaga mayai na kumueleza kuwa ametotoa watoto wa nyani, kunadhihirisha kuwepo kwa usemezano kwa kupitia kipengele cha kronotopu.

**Utendaji**

Utendaji ni kipengele cha usemezano ambacho kinaruhusu utagusano wa kisemezano katika utendaji ulio katika mjadala. Kwa mujibu wa Bakhtini (1986), utendaji ni mbinu moja wapo ya lugha; ni namna ya kuzungumza. Mshairi anastahili kuvutia hadhira yake kwa kunasa fikra zao kabisa. Hadhira lazima iwe makini ili ipate kusikia na kutekeleza. Ubeti mmoja na mwingine huunganishwa kwa kutumia urudiaji au uradidi, utumiaji wa ishara na kiimbo kwa kupandisha sauti na kushusha sauti ili kuivutia hadhira yake, hutumia toni ya shairi. Toni hiyo inawezakuwa ni kwa njia ya kejeli, chuki, huzuni na kushawishi. Msanii wa *Kimbunga* ametumia usemezano wa utendaji kwa kurudia maneno ya uradidi ya kujitawala. Mfano katika shairi la *Kujitawala* katika ubeti wa kwanza.

1. *Kujitawala ni kwema, kuliko kutawaliwa*
   *Kujitawala ni umma, kila yao kuamuwa*
   *Kujitawala si kama, ulanguzi na rushuwa*

Kupitia shairi hili, msanii ametumia usemezano wa utendaji wa kurudia maneno katika kila ubeti, neno la ***kujitawala*** limerudiwa na msanii katika shairi hilo. Kupitia uradidi huo, ndio tunapata usemezano wa utagusano wa kimawazo, kwani hadhira anapolirudia neno moja mara kwa mara humpelekea katika utendaji uliomo katika mjadala wa kififkra.

**Usimulizi wa Kisanaa**

Kipengele kingine cha usemezano kilichotumiwa na msanii wa diwani ya *Kimbunga* ni usimulizi wa kisanaa, ambapo msanii hutumia nafasi ya kutumia utanzu mwingine wa fasihi simulizi kwa njia ya usemezano wa masimulizi. Msanii hutumia hadithi au kisa fulani kwa njia ya masimulizi. Na hapo huonekana msanii anasimama kama fanani/mtambaji wa hadithi wakati wa kutoa shairi lake, na wasomaji husimama kama wasikilizaji/hadhira wakisilikiza na kuipokea hadithi. Katika usimulizi wa kisanaa, sauti neni ni muhimu sana kwa hapo na husimamiwa na mshairi kwa kutumia nafsi ya kwanza ili kuweza kuonesha kuwa hadithi au kisa kuwa kinasimuliwa na yeye. Kipengele hiki kimetumika katika shairi la *Kibwangai* katika ubeti wa kwanza.

1. *Kuna hadithi ya kale, kwa babu nimepokeya*
   *Kwa manyani zama zile, mkasa ulitokeya*
   *Nilikuwa mwanakele, hayo nikazingatia*

*Leo nawadokezeya, kwa nilivyoyafahamu*

Kupitia data hii, inaonesha kuwa msanii wa diwani ya *Kimbunga* ametumia usemezano katika diwani yake kwa kuingiza usimulizi wa kisanaa katika mashairi yake. Usemezano huu unakuja pale msanii anapoanza kusimulia hadithi kwa njia ya shairi. Aliposema '***Kuna hadithi ya kale, kwa babu nimepokeya'.*** Hapa mshairi huwa anasemezana na msomaji ambaye anakuwa ni hadhira wa hadithi inayosimuliwa na msanii. Aidha, usemezano huu pia unaingia katika usemezanoghaibu kwa wasimuliwa hadithi kwa huwa hawaonekani wala hawajulikani.

**Kani Pewa na Kani Kitovu**

Katika vipengele vya usemezano, kuna na kani pewa na kani kitovu. Ambapo kani pewa ni sifa ya utunzi fulani ambao unaweza kubadilika katika mpito wa wakati huu tulionao. Aidha, kani kitovu ni sifa ya utunzi fulani ambayo huwa haibadiliki. Katika diwani hii ya *Kimbunga* usemezano wa aina hii haukudhihiri kwa msanii huyu.

**Sajili mbalimbali**

Sajili mbalimbali ni kipengele kimojawapo cha usemezano, ambapo msanii hutumia sajili nyingine au tunaweza kusema, ni kutumia maandiko mengine yaliyo nje ya utanzu wa fasihi husika, na kuyaingiza katika kazi ya kisanaa. Sajili hizo ni kama sajili ya magazeti, sajili ya sheria, sajili ya mazungumzo, na sajili ya biashara. Yaani, inaeleza juu ya matukio yalivyotokea. Kama vile sajili ya biashara, ikazungumzia matukio ya pale dukani namna muuzaji anavyozungumza na mnunuzi (msimuliaji). Katika diwani hii msani ametumia usemezano wa sajili ya hadithi ya mkutano wa wanyama wanavyosemezana. Mfano shairi la *Kibwangai* katika ubeti wa 5 na 6.

5. *Pana mmoja kasema, kibwangai kumwambia*
*Kama tutalokutuma, weza kututimiziya*
*Isiwe kurudi nyuma, ewe mwenzetu sikia*
*Wewe tumekuchagua, utumikiye kaumu*

*6. Kibwangai akasema, hayo nimezingatiya*
*Kidete nitasimama, jitihada kutumiya*
*Kwa kusia na kulima, mpate jifaidiya*
*Sitobadili mawazo, ilipwe yangu kaumu*

Kupitia shairi hili, msanii amedhihirisha kutumia usemezano katika kipengele cha sajili mbalimbali. Kwa kutumia sajili ya mazungumzo ya wanyama kupitia utanzu wa hadithi, na kuonesha namna wanyama wanavyosemezana katika mazungumzo yao, kwa kusema mmoja wao na mwengine kuitikia au kujibu. Mfano ni pale mnyama mmoja alipomwambia mwenziwe '***Pana mmoja kasema, kibwangai kumwambia…'*** na yule Kibwangai naye akajibu '***Kibwangai akasema, hayo nimezingatia…'***. Hivyo imedhihirika kuwepo kwa usemezano wa kipengele cha sajili ya mazungumzo ya wanyama.

**Hitimisho**

Makala haya imechunguza usemezanoghaibu unaojitokeza katika diwani ya *Kimbunga,* ili kuweza kubaini ni kwa kiasi gani nadharia ya usemezano inavyoweza kujitokeza katika utanzu wa mashairi na namna inavyoweza kwenda mbele kwa kuibua dhana mpya ya usemezanoghaibu. Kinyume na alivyosema muasisi wa nadharia hii. Uchunguzi umebaini kuwa katika mashairi, kunakuwapo usemezano. Usemezano huo unaweza kuwa ni wa mtu mwenyewe binafsi, mtu na mtu mwengine, na hata usemezano wa mshairi mmoja na mshairi mwengine. Aidha, uchambuzi umeweza kubaini kuwepo kwa usemezanoghaibu. Makala imeshugulikia usemezano wa diwani moja tu, na wala haikugusia upande wa diwani nyengine. Na hilo litakuwa eneo jengine la kitaaluma linalohitaji kufanyiwa utafiti ili kuweza kuipima vyema dhana hii ya usemezano katika mashairi, hasa dhana hii mpya ya usemezanoghaibu.

**Marejeleo**


Bakhtin, M. M. (1981). *The Dialogic imagination: Four Essays.* Austin: University of Texas Press.

Bakhtin, M. M. (1984). *Rabelais and His World Bloomington:* Indiana University Press.

Baraza la Kiswahili Zanzibar BAKIZA. (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha.* Nairobi: Oxford University Press.

Biersteker, A. M. (1996). *Kujibizana*. Poetic Dialogue as Political Action. East Landing: Michigan State University.

Haji Gora, H. (1994). *Kimbunga.* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Hassan, A. M. A. (2013). 'Kuchunguza Vipengele vya Fani katika Mashairi ya Kiswahili: Ulinganishi na Ulinganuzi wa Mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji'. Chuo Kikuu Huria. Tanzania.

Mohamed, S. A. (1980). *Sikate Tamaa.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Mtimbo, A. na Suleiman, K. (2004). 'Uhakiki wa Diwani ya *Kimbunga'.* Utafiti Mdogo wa Kukamilisha Masharti ya Shahada ya Kwanza. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mukarovsky, J. (1977). *The World and Verbal Art:* Selected Essays. New Haven University Press.

Mwita, C. (2018). Matumizi ya Usemezano katika Tamthiliya ya Kiswahili: Ulinganisho wa *Mashetani* na *Pambo.* Tasnifu ya Umahiri. Chuo Kikuu cha Dodoma. Tanzania.

Njogu, K. (1993). *Dialogic Poetry: A Contestation and Social Challenge in East Africa Poetic Genres.* PhD Dissertation. Yale university.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1994). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Suter, D. J. (2017). Usemezano katika Diwani ya *Sikate Tamaa.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi. Focus Publications Ltd.